

Mradi wa Udhubiti Uvuvi na Maendeleo shirikishi Kusini Magharibi ya Bahari ya Hindi (SWIOFish)

Katika kuimarisha usimamizi madhubuti wa uvuvi ngazi ya kikanda, kitaifa na kijamii Serikali inatekeleza Mradi wa Udhubiti Uvuvi na Maendeleo shirikishi Kusini Magharibi ya Bahari ya Hindi (SWIOFish).

Mradi huu unatekelezwa katika maeneo ya Pwani ya Bahari ya Hindi kwa upande wa Tanzania Bara na katika wilaya zote 10 upande wa Zanzibar pamoja na Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu (EEZ) ambapo watekelezaji wakuu ni Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi (Tanzania Bara), Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Zanzibar) na Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu.

Mradi huu umefanikisha kuanzishwa kwa mfumo wa ukusanyaji na uhifadhi wa takwimu za uvuvi na mtandao wake kwa ajili ya wananchi kujipatia taarifa za uvuvi kwa muda husika (SAMAKI Information System) na kupatikana kwa mpango mkuu wa miaka 15 wa Usimamizi na Uendelezaji wa Uvuvi (Zanzibar Fisheries Masterplan).

Mafanikio mengine ni kuendelea kudhamini masomo ya Ngazi ya Uzamili na Uzamivu katika fani ya Uvuvi (Wanafunzi watano ngazi ya Uzamili (Masters) na wanafunzi watatu katika ngazi ya Uzamivu (PhD).

Mradi huu ulianza utekelezaji wake Juni 22, 2015 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Septemba 30, 2021.